

TaCRI

TAASISI YA UTAFITI WA KAHAWA TANZANIA

# Taarifa ya Mwaka 2003

# Yaliyomo


| | | Uk. |
|---|---|---|
| | Ujumbe wa Mwenyekiti na Mkurugenzi | 1 |
| 1 | Maelezo kuhusu TaCRI | 3 |
| 2 | Mkakati wetu wa Miaka Mitano | 6 |
| 3 | Shughuli za Menejimenti | 8 |
| | Fedha na Utawala | 9 |
| 4 | Uboreshaji wa Zao | 10 |
| 5 | Tija ya Zao na Usindikaji wa Mwanzo | 12 |
| 6 | Virutubisho vya Zao | 13 |
| 7 | Riziki na Uhakika wa Kipato | 15 |
| 8 | Usambazaji wa Teknolojia na Mafunzo | 16 |
| 9 | Uchunguzi Kifani | 18 |


*Picha ya Jalada la mbele: Aina mpya ya kahawa zisizoshambuliwa na magonjwa, zinazotoa mavuno mengi zinazozalishwa kwa vikonyo.*



**Bw. Edwin I. M. Mtei**
*Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi*
*Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania*

Inanipa faraja kubwa kuandika dibaji hii kwa ajili ya Taarifa ya Mwaka ya TaCRI nikiwa Mwenyekiti wa kwanza wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi hii mpya. Taarifa hii ya kwanza ya mwaka ni hatua kubwa inayotoa, kwa muhstasari, shughuli za Taasisi na mafanikio yake tangu ianze rasmi.

Wadau wa kahawa wana matarajio makubwa sana kutoka TaCRI. Ninajivunia mafanikio yaliyopatikana hadi sasa. Nina imani TaCRI itatimiza wajibu wake na kuchangia katika kazi kubwa ya kufufua tasnia ya kahawa Tanzania. TaCRI imeanza vizuri. Hii inanipa matumaini makubwa kwa siku zijazo.

Tumepata misaada ya kutosha kutoka kwa wadau kwa ajili ya kuanzisha TaCRI. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa serikali ya Tanzania na Muungano wa nchi za Ulaya kwa misaada yao ya nyenzo, fedha na kutuunga mkono sasa na miaka ijayo wakati wa kutekeleza mkakati mpya wa muda wa kati.

Edwin I.M. Mtei
Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi



**Profesa James M. Teri**
*Mkurugenzi Mtendaji Mkuu*
*Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania*

Ninayo furaha kuwakaribisheni kwenye Taarifa hii ya TaCRI ya Kwanza ya Mwaka.

TaCRI iliandikishwa mwaka 2000 na kuanza kazi rasmi September 2001 kuchukua nafasi ya ile taasisi ya serikali ya utafiti wa kahawa na kuweka mkazo katika dhima ya wadau na utafiti unaokidhi mahitaji. Tunalo lengo moja kubwa kuhusisha tasnia ya kahawa Tanzania iwe na ustawi endelevu kwa ajili ya kuboresha maisha ya wazalishaji wa kahawa na kuifanya Tanzania kuwa muuzaji muhimu wa kahawa bora ya wingi wa kuridhisha kwenye soko la dunia.

Taarifa hii ya Mwaka ni hatua muhimu ya kufikia lengo letu. Ina ainisha shughuli na mafanikio ya Taasisi tangu ianzishwe na Mpango wake wa Utekelezaji wa Miaka Mitano, 2003-2008 wa kufufua na kuendeleza tasnia ya kahawa Tanzania iwe na manufaa endelevu.

TaCRI na wote tunaofanya kazi kwenye taasisi tunawajibika kwenu nyinyi wadau wetu. Tafiti zote za kahawa na usambazaji wa matokeo ya tafiti hizo umebuniwa kwa makini ili kuhakikisha kuwa unawanufaisha na kukidhi mahitaji ya wakulima mbalimbali wa

kahawa katika kanda tofauti nchini kote. Kwa kuzingatia hili, tumekuwa makini katika kuhakikisha kuwa Mkakati wa Mpango wa Utekelezaji umetayarishwa kwa kushirikisha wadau kikamilifu.

Kwa kuwa hii ni taarifa yetu ya kwanza ya mwaka, tumetenga nafasi katika kurasa hizi ili kuelezea maadili na malengo yetu ya msingi na kuorodhesha mafanikio tuliokwishapata tangu TaCRI ianze kazi na malengo tuliyonayo kwa miezi kumi na mbili ijayo. Mnaweza kupima mafanikio yetu katika taarifa yetu ya mwaka ujao.

Kwa hakika, nimefarijika sana na mafanikio yetu mpaka sasa, ukizingatia kwamba kwa miaka miwili iliyopita Kituo cha Utafiti, Lyamungu tulichorithi kilikua kwenye hali mbaya sana.

Tayari, kutokana na msaada wa STABEX na ushuru kwenye kahawa, tumeanza kufanya ukarabati, kuajiri timu za wataalamu, wanasayansi wenye juhudi na kuendeleza uhusiano wa kikanda na kimataifa ili kuharakisha maendeleo yetu ya utafiti. Aidha, tumebainisha aina mpya 36 za kahawa mahuluti ambazo zinaonyesha matumaini katika utoaji wa mavuno mengi, kutoshambuliwa na magonjwa na kua na muonjo mzuri. Tunatarajia kwamba kufikia mwaka 2007 tutakuwa tukizalisha na kusambaza vipandikizi milioni 5 vya aina mpya za kahawa. Majadiliano na CIRAD yanaendelea ili kupata teknolojia yao kwa ajili ya uzalishaji kwa wingi na usambazaji wa aina bora mahuluti.

Kwa mwaka huu, TaCRI itaonekana kwa uwazi zaidi katika tasnia, tunapoanza kuchapisha na kusambaza matokeo ya kwanza ya utafiti kwa vipeperushi na miongozo mingine ya kitaalamu. Miongoni mwa mambo mengine mengi, tutapanua pia mpango wa mafunzo kwa wakufunzi na kuendelea na majaribio ya shambani ya aina mpya bora za kahawa

Tunapenda kuwakaribisha kwa moyo mkunjufu makao yetu makuu yaliyopo Lyamungu, Moshi au vituo vya kanda vilivyopo Maruku, Bukoba; Mbimba, Mbozi na Ugano, Mbinga. Tunakaribisha maoni na ushauri kuhusu namna ya kuboresha utoaji wa huduma za TaCRI au vipengele vingine kwenye tasnia ya kahawa.

Nawatakia kila la heri kwa msimu ujao.

Profesa James M. Teri
Mkurugenzi Mtendaji Mkuu
Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania

# TaCRI ni nini?

Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI) ilisajiliwa mwaka 2000 na kuanza kazi kisheria September 2001 kwa lengo kubwa la kufufua tasnia ya kahawa Tanzania, kwa kuweka mkazo katika dhima ya wadau na mahitaji ya soko na kulenga dhana ya **UTAFITI KWA MAENDELEO!**

Taasisi itatoa huduma muhimu kwa wadau wa tasnia ya kahawa hapa nchini kwa kuwapatia teknolojia mwafaka inayofaa na kutekelezeka na ushauri kuongeza tija na ubora wa kahawa. Matokeo ya haya yote ni ongezeko la faida na ubora wa maisha kwa wazalishaji wa kahawa na kuongeza ushindani wa kahawa ya Tanzania katika soko la dunia.




*Biashara ya zao la kahawa ni shughuli muhimu*

**Umiliki**

TaCRI inamilikiwa na wadau wanaohudumiwa. Hawa ni pamoja na: Wazalishaji wadogo na wakubwa wa kahawa, vyama vya ushirika vinavyohusika na kahawa, wasindikaji wa kahawa, wafanyabiashara wa kahawa, asasi zisizo za kiserikali (AZISE) sekta binafsi, na serikali.

**Ugharamiaji**

TaCRI ni asasi isiyo ya kibiashara. Taasisi inapata mapato yake kutokana na michango ya wanachama wake kupitia ushuru, michango ya serikali na wafadhili, shughuli za kushirikiana, pamoja na mauzo ya nyenzo na huduma (mfano mbegu na machapisho).

TaCRI kama taasisi mpya, ina mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati mkubwa unaohitajika pamoja na kununua vifaa vipya kwa ajili ya kuiinua taasisi iweze kufanya kazi kwa ufanisi. Sehemu kubwa itatolewa na Muungano wa Ulaya kuiwezesha taasisi kutekeleza Mpangao wake wa Miaka Mitano.

TaCRI itanufaika pia na riba kutokana na fedha za STABEX zitakazowekwa kwenye akiba maalumu.

# Mtazamo wa TaCRI



*TaCRI inaendeleza aina mpya ya kahawa inayotoa mavuno mengi na isiyoshambuliwa na magonjwa.*

Ili asasi au biashara yoyote iweze kufanikiwa ni muhimu kuwa na mtazamo ulio wazi utakaowezesha kupanga shughuli na kupima mafanikio.

TaCRI ilipoanza kazi rasmi Septemba 2001, kazi ya kwanza ya timu ilikuwa ni kutayarisha Mtazamo wa Taasisi. Kwa kutumia mchakato wa pamoja uliojumuisha wafanyakazi wote wa Taasisi tulipata seti ya maadili na malengo yatakayokuwa msingi wa usimamizi na utendaji kazi wa TaCRI.

**Maadili yetu**
TaCRI inaazimia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maadili makuu yafuatayo:-

- Utoaji na usambazaji thabiti wa teknolojia kwa kadiri ya mahitaji na ambao unakidhi haja ya wadau na wenye mtazamo wa kisoko.
- Uongozi ulioelimika
- Utendaji kazi bora na wa kiwango cha juu
- Kuwa na hali ya uharaka
- Kuheshimiana na kuaminiana baina ya watumishi wa ngazi zote
- Utambuzi wa gharama
- Kufanya kazi pamoja "bega kwa bega"
- Kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya wazalishaji wa kahawa.

**Dira yetu**
Dira ya TaCRI ni kuchangia katika kuboresha tasnia ya kahawa Tanzania iwe na ustawi endelevu.

**Jukumu letu**
Taasisi itafikia dira hii kwa kuendeleza na kueneza teknolojia mwafaka ili kuinua tija ya kahawa ndani ya muundo mzuri wa sera. Matokeo tarajiwa ni kuongeza ushindani wa kahawa ya Tanzania katika soko la dunia na hatimaye kuongeza kipato, kupunguza umaskini na kuboresha maisha ya wazalishaji wa kahawa.


**Lengo letu**
Lengo la TaCRI ni kuanzisha tasnia ya kahawa yenye manufaa na endelevu katika Tanzania.

**Kufikia lengo letu**
TaCRI itafanya kazi zake kwa kufuata vigezo vifuatavyo:

- Kufanya kazi kwa karibu na wadau wote wa kahawa ili kuwa na mtazamo mmoja wa kile kitakachowezekana.
- Kusimamia kwa njia inayofaa na kwa ufanisi rasilimali ili kukidhi mahitaji ya wadau.
- Kujitahidi kuwa na taasisi ya utafiti yenye usimamizi thabiti, uwezo kifedha, ufanisi bora inayoona mbali na ambayo inajulikana kitaifa na kimataifa.

- Kuvutia, kutoa motisha na kuwa na timu ya wanasayansi bora, wataalamu wengine na watumishi wasaidizi.
- Kuwa makini katika uendelezaji wa teknolojia ambayo inalenga katika kutatua matatizo yaliyopo na yatakayojitokeza katika tasnia ya kahawa.
- Kuhakikisha kuwa uvumbuzi utakaopatikana unafikishwa haraka na kwa ufanisi kwa walengwa.
- Ufuatiliaji wa mara kwa mara na kuangalia upya maendeleo na mafanikio.

## Muundo wa TaCRI



# Ufafanuzi wa Mkakati Wetu wa Miaka Mitano: 2003-2008

## Mkakati wa Mpango wa Utekelezaji

Kazi ya kwanza ya TaCRI ya kipaumbele muhimu iliyofanikiwa vizuri ni utayarishaji wa Mkakati wa Mpango wa Utekelezaji wa Muda wa Kati (Miaka Mitano) wa utafiti na maendeleo unaozingatia mahitaji ya wadau.

Madhumuni ya kuweka mkakati huu muhimu ilikuwa ni kutengeneza muundo wa kiutendaji wa TaCRI. Mkakati huu usingetengeneza tu muundo wa taasisi hii mpya, bali ungetoa pia mpango wa utekelezaji na bajeti ya miaka mitano ya mpango wa utafiti na maendeleo ili kufufua tasnia ya kahawa Tanzania. Mkakati wa Utekelezaji utakuwa alama teule kuonyesha pale TaCRI itakapofikia malengo yake na ahadi zake kwa wadau.

**Utekelezaji kwa Awamu tatu**
Mkakati wa Mpango wa Utekelezaji ulitekelezwa kwa awamu tatu, katika mwezi Julai/Agosti na Septemba 2002, na Januari 2003. Kazi ilifanywa na wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Cranfield cha huko Uingereza kwa ushirikiano wa Mkurugenzi Mtendaji na wafanyakazi wa TaCRI.

Awamu ya Kwanza ilijumuisha uchanganuzi wa wadau nchi nzima, na Warsha kwa wadau ambapo katika kipindi hicho shughuli kuu za kipaumbele ambazo zingefanywa na TaCRI zilibainishwa na wadau.

Katika awamu ya Pili, tafiti za nyuma na zile zilizokuwa zinaendelea zilipitiwa upya na muundo wa TaCRI ulitengenezwa. Mahitaji ya mafunzo na utafiti ili kusaidia taasisi kufikia malengo yake yalitathminiwa; aidha faida ambazo tasnia ingepata kwa TaCRI kushirikiana na asasi nyingine kitaifa, kikanda na kimataifa pia zilifikiriwa.

Katika awamu ya mwisho, mpango mpana wa muundo wa utendaji kazi wa TaCRI ikiwa ni pamoja na matokeo yake mahsusi, utekelezaji na muda wa utekelezaji kwa kila idara miongoni mwa idara tano, kama ilivyoelezwa katika awamu ya pili ulitayarishwa. Hii ilijumuisha mpango wa utekelezaji kwa idara zote na bajeti pana kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Hatua ya mwisho ilikua Mkakati wa Mpango wa Utekelezaji kupitishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 20 Januari 2003.

**Kukidhi Mahitaji ya Wadau**
Mahitaji ya utafiti wa kitaalamu yaliyobainishwa na wadau katika Mkakati wa Mpango wa Utekelezaji yalikuwa: kuendelea kutoa na kusambaza aina bora za kahawa zinazotoa mavuno mengi, zisizoshambuliwa na



Uchanganuzi wa wadau

magonjwa (zote Arabika na Robusta), pamoja na kuzizalisha kwa wingi na kuzisambaza vizuri kwa wakulima kuzitathmini katika mifumo mbalimbali ya uzalishaji kahawa (maeneo ya ikolojia); mifumo jumuishi ya gharama nafuu ya kudhibiti wadudu waharibifu, udhibiti wa virutubisho vya kioganiki na visivyo vya kioganiki ikiwa ni pamoja na utoaji wa huduma za uchanganuzi wa udongo na majani (kibiashara) na teknolojia ya usindikaji wa mwanzo ambayo inafaa kwa matumizi ya ngazi ya shamba. Matokeo yatakuwa ni kupunguza gharama za uzalishaji, kuongeza tija na ubora ili kuifanya kahawa ya Tanzania kuwa na ushindani na hatimaye kuongeza pato na faida.

Usambazaji teknolojia na mafunzo umeonekana kama shughuli muhimu ya TaCRI kama Tanzania itachukua tena nafasi yake na kurudisha sifa ya kuzalisha kahawa bora kwa wingi. Kutoka makao makuu Lyamungu Mkoani Kilimanjaro, TaCRI itahudumia nchi nzima kupitia vituo vyake vya kanda Mbimba, Wilaya ya Mbozi na Ugano, Wilaya ya Mbinga kwa upande wa Kusini na Maruku, Wilaya ya Bukoba kwa upande wa Magharibi.

Vilevile, kuna umuhimu wa kuelewa na kuelezea uchumi wa uzalishaji na usindikaji wa kahawa ili kuwavutia waundaji sera kusaidia upatikanaji wa masoko na kuelewa maisha na kipato cha kaya za wakulima wa kahawa ili kuhakikisha kwamba utafiti ni mwafaka kwa mahitaji yao. TaCRI itabainisha na kuweka kipimo cha chini cha shamba linalofaa kiuchumi, na kubainisha njia za kuboresha mapato ya wakulima kutokana na kilimo cha kahawa. Hii inaweza kujumuisha uanzishaji wa vikundi zaidi vya wakulima ili kushirikiana rasilimali. Dhima ya mikopo katika upatikanaji wa pembejeo kama vile mbolea ni suala jingine ambalo linahitaji kufanyiwa utafiti.

Kwa kifupi, eneo hili la utafiti linaweza kufupishwa chini ya kichwa cha habari "Uhakika wa Kipato" kuelezea mahitaji ya kufanya utafiti utakaolenga maisha yanayoendeshwa kwa fedha na siyo teknolojia tu ambayo wakulima wanaweza au kutoweza kuimudu. TaCRI itashawishika na mahitaji haya ijapokuwa haikuwa kawaida hapo zamani kuiweka katika udhamini wa taasisi za utafiti wa mazao wa jadi.



*Ukataji mkali unatakiwa ili kurekebisha majaribio ya utafiti yaliyotelekezwa*

# Shughuli za menejimenti

Wajibu wa Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya juu ya TaCRI ni kuhakikisha kwamba inaanzishwa taasisi ya utafiti wa kahawa yenye usimamizi mzuri, inayojitegemea kifedha, inayojali wadau wake, inayoona mbele, inayoheshimika na ambayo ni endelevu.

Timu ya menejimenti ina wajibu wa kuchukua hatua za kisera na kufanya marekebisho ili muundo wa taasisi uwe mzuri zaidi na kuajiri wataalamu wenye ubora wa hali ya juu. Kwa ujumla, menejimenti ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za kila idara katika taasisi ili kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanaenezwa kwa ufanisi na kwa wakati unaotakiwa, na kuhakikisha kuwa utafiti unazingatia yale masuala yanayohitaji kufanyiwa utafiti ambayo yanahusiana na kahawa ya Tanzania na wakulima wa kahawa wa Tanzania.

**Mafanikio Makuu 2001-2003**

- Mkakati wa Mpango wa Utekelezaji ulitayarishwa kwa ushirikiano mkubwa na wadau. Ulipitishwa na Bodi ya TaCRI mwezi Januari 2003. Hatua za kuridhisha zimefikiwa ili kuanza kutekeleza mkakati.
- Msaada wa EU/STABEX ulipatikana kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza shughuli za TaCRI.
- Warsha mbili za TaCRI kwa ajili ya kujenga timu zilifanyika mwaka 2002. Lengo lake lilikuwa kuendeleza na kuimarisha moyo wa kufanya kazi kitimu “bega kwa bega” miongoni mwa wafanyakazi na kutafakari maadili ya pamoja katika TaCRI.
- Shamba la utafiti la Lyamungu limefanyiwa ukarabati kwa kiasi kikubwa. Majaribio mengi ya utafiti yaliyorithiwa na TaCRI yalikuwa kwenye hali isiyoridhisha. Haya yamefanyiwa marekebisho ili majaribio yaweze kuendelea tena kukusanya data zenye manufaa.
- Wataalamu wa TaCRI kutoka fani mbalimbali walishiriki kwenye safari za mafunzo na warsha mbalimbali ndani na nje ya nchi.
- Kukamilisha ajira za wafanyakazi wote inaendelea vizuri
- Tathmini ya awali ya nyenzo za TaCRI kwa ajili ya ukarabati yamekamilika.
- Ukosefu wa vitabu vya kisasa vya Wanasayansi wa TaCRI ni tatizo kubwa kwa utafiti thabiti. Ili kutatua tatizo hili, Taasisi imeingia mfumo wa upataji Habari za Muhimu za Kielektroniki za Maktaba ya Kilimo (TEEAL) na imejiunga na Mpango wa Kuendeleza Taarifa za Utafiti (PERI). Hii kwa pamoja imeipa

TaCRI uwezo mzuri wa kielektroniki wa kupata majarida na tafiti za kisasa.

**Vipaumbele Vikuu 2003-2004**

- Kukamilisha kuajiri wafanyakazi wenye ubora wa hali ya juu
- Kuendelea kubadili na kuboresha utamaduni wa kazi kulingana na maadili ya taasisi.
- Kuanza kufanya ukarabati wa makao makuu ya Lyamungu, vituo vya kanda na kuanza mchakato wa tenda za ununuzi wa vifaa vya kuanzia.
- Kupitia upya Vipengele vya kusajili TaCRI na Vipengele vya kushiriki na kutoa ushauri wa kurekebisha Sheria ya Kahawa kama itakavyoonekana.

# Fedha na Utawala



*Dkt. Omar Kizango*
*Mkuu wa Idara*

**Mafanikio Makuu 2001-2003**

- Kutayarisha nyaraka za utawala, utumishi na fedha .
- Kusimamia uhakiki mali uliyofanywa na Bodi ya Ukaguzi iliyoteuliwa na serikali ili kuwezesha makabidhiano na TaCRI.
- Kuboresha mawasiliano katika Kituo cha Lyamungu na sehemu za nje.
- Kufanya ukarabati, na matengenezo ya mara kwa mara ya mashamba.
- Kuimarisha ulinzi katika kituo cha Lyamungu.
- Kuwapanga upya kwa ufanisi 50% ya watumishi wa zamani waliorithiwa na TaCRI kutoka serikalini.

**Vipaumbele Vikuu 2003-2004**

- Kukopyutisha mfumo wa uhasibu na kuboresha ujuzi wa teknolojia ya mawasiliano (IT).
- Kuanzisha na kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Habari (MIS).


# Idara ya Uboreshaji wa Zao



Bw. Deusdedit Kilambo, Kaimu Mkuu wa Idara

Mojawapo ya vikwazo katika tija, maendeleo na ustawi wa tasnia ya kahawa hapa Tanzania ni kuendelea kulima aina za kizamani ambazo hutoa mavuno kidogo na zinashambuliwa sana na magonjwa, kutu ya majani (CLR) na chulebuni (CBD). Moja kati ya madhumuni makubwa ya TaCRI ni kubainisha aina inayotoa mavuno mengi na isiyoshambuliwa na CLR na CBD, pia yenye matunda makubwa na muonjo mzuri na kustawi vizuri kwenye maeneo tofauti yanayozalisha kahawa hapa Tanzania.

Wajibu wa Idara ya Uboreshaji wa Zao ni kuendeleza na kutoa aina mpya za kahawa za Arabika na zinazotoa mavuno mengi, zisizoshambuliwa na magonjwa, zenye punje kubwa



Bw. Damian Mtenga, Utafiti wa kahawa kwa vitendo

na muonjo mzuri. Aina hizi mpya zitazalishwa kwa wingi kwa miaka mitano kwenye pragramu kabambe ya taifa ya kupanda kahawa upya inayotarajiwa kuanza 2007. Mpango wa kutoa aina bora za kahawa utaimarishwa kwa kuteua wataalamu wapya kwenye taaluma hii wenye uzoefu pamoja na misaada ya kitaalamu ya kikanda na kimataifa.



Juu: Jaribio lilokarabatiwa
Kulia: Shamba lililotelekezwa, Lyamungu



**Mafanikio Makuu 2001-2003**

- Aina 36 zenye matumaini ya ubora wote unaotakiwa zimebainishwa. Majaribio yanaendelea kupata aina zinazoonyesha kiwango cha juu cha sifa zote zinazotakiwa.
- Aina mahuluti 20,000 zilizalishwa kupitia ustawishaji wa tishu huko Ufaransa. Hizi zinafanyiwa tathmini kwenye mashamba mbali mbali nchini ili kuona ubora wake.
- Sampuli 35 za aina bora zilipelekwa nchini Kenya kufanyiwa tathmini ya muonjo. Sampuli zote 35 zilipimwa katika ubora wakusafirisha nje (FAQ); 57% ya sampuli zilipimwa katika daraja la kati na zenye kiwango cha kati na cha juu cha asidi, na 74% ya sampuli zilizopelekwa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) zilikuwa katika madaraja bora ya 5-6. Kazi ya kuthibitisha matokeo haya, ikijumuisha majaribio ya muonjo wa sampuli nyingine zaidi inaendelea.
- Miti ya kahawa 1482 ilichambuliwa juu ya kustahimili kutu ya majani kuanzia Septemba 2001, ambapo 2% tu ilionekana kuathiriwa na kutu ya majani. Majaribio yanaendelea.
- Miti ya kahawa 433 ilichambuliwa katika maabara ili kubaini ustahimilifu wake kwa CBD, ambapo 13% ilionekana kustahimili CBD
- Tathmini ya mlolongo wa majaribio ya aina 16 zilizopandwa katika maeneo tofauti yanayostawisha kahawa nchini zimeonyesha kuwepo kwa aina nyingine mahuluti zenye ubora wa kuridhisha zinazoweza kutolewa pia kwa wakulima siku za usoni.
- Aina bora sita za Robusta zilizochaguliwa kutoka katika mashamba ya wakulima chini ya STABEX mwaka 1995 na kutolewa 1996 zipo katika uzalishaji wa kiuoto katika vitalu vya kuzalishia (VPU) huko Kagera. Kumekuwa na udhaifu katika uchukuaji wa miche kutokana na kuvunjika moyo kwa wakulima kutokana na bei ndogo ya kahawa kwenye soko. Kwa sasa mahitaji ya aina hizi yameongezeka kutokana na kuongezeka kwa bei kidogo misimu ya karibuni na kufanya paendelee kuwepo na haja ya kuzalisha mimea ya kupanda.
- Utafiti mpana umefanywa kuthibitisha mtawanyiko wa kijiografia wa ugonjwa wa mnyauko fusari (CWD) nchi nzima. Robusta pekee ndiyo inayoathirika na CWD. CWD ni tishio kwa tasnia ya kahawa ya Robusta katika mkoa wa Kagera. Mapendekezo ya awali ya kuzuia uenezaji zaidi wa ugonjwa yanaenezwa

**Vipaumbele Vikuu 2003-2004**

- Kuajiri mzalishaji wa mimea kuchukua nafasi ya Mkuu wa Idara ya Kuboresha Kahawa na kuingia mkataba na wataalamu wa nje waliobebea kwenye eneo hili kusaidia.
- Kukarabati mashamba yote ya majaribio na kuanza kuyastawisha upya kwa kuboresha utunzaji na utumiaji wa pembejeo
- Kukarabati vitalu na vyumba vya kukomazia vikonyo.
- Kukarabati na kuandaa maabara ya patholojia ya mimea na chumba chenye hali joto inayodhibitiwa.
- Kuanzisha kwa majaribio ya kimaabara ya ustawishaji wa tishu kuangalia uwezo wa miti iliyochaguliwa kwa ajili ya kuzalishia kwa njia ya uanzishaji vinitete kwa kutumia selimwili.
- Kuendelea na uchaguzi wa aina ya Robusta ambazo zinastahimili ugonjwa wa CWD.

# Tija na Usindikaji wa Mwanzo wa Zao



*Dkt. Grace Chipungahelo, Mkuu wa Idara*

Kiini cha mafanikio ya baadaye katika tasnia ya kahawa katika Tanzania ni kuongeza tija kwa eneo au kwa mti kutegemea mfumo wa ukulima, kupunguza gharama za uzalishaji na kuendeleza ubora wa kahawa katika ngazi ya usindikaji wa mwanzo.

Kazi za Idara ya Tija na Usindikaji wa Mwanzo ni kusaidia mpango wa taifa wa ufufuaji na upandaji upya wa kahawa kwa kufanya thabiti wa ukulima wa zao na udhibiti wa wadudu waharibifu katika mifumo mbalimbali ya ulimaji wa kahawa Tanzania. Idara pia itatoa taarifa na kufanya utafiti juu ya teknolojia za usindikaji wa mwanzo na kutoa data za hali ya hewa.

**Mafanikio Makuu 2001-2003**

- Utafiti wa nyuma juu ya njia bora za utunzaji wa zao na udhibiti wa wadudu waharibifu umepitiwa upya na Idara hii. Taarifa hizi zinatayarishwa katika seti za ujumbe wa kitaalamu kutengeneza chapisho zitakazosambazwa kwa wakulima mwaka 2003/4.
- Bustani Botania imeanzishwa Lyamungu kukusanya aina za mimea yenye uwezo wa kuthibiti wadudu waharibifu wa kahawa. Hii imejumuisha mimea ambayo wakulima wamebaini kuwa ina uwezo ya kiuadudu. Kwa sasa utupa na mwarobaini imethibitika kuwa na uwezo wa kiuadudu.

**Vipaumbele Vikuu 2003 – 2004**

- Kukamilisha uandaaji na uchapishaji wa taarifa za kitaalamu kuhusu aina mbalimbali zilizopo za utunzaji wa zao na mbinu za udhibiti wa wadudu waharibifu kwa ajili ya kuzitawanya kwa wakulima.
- Kuanza majaribio ya kubaini msongamano wa mmea wenye matumaini na utaratibu wa upogoaji wa matawi kwa aina mpya ya kahawa, kuwapa wakulima ushauri wa mchanganyiko mzuri katika mifumo mbalimbali ya ukulima (pamoja na kupanda mseto na migomba).
- Kuanzisha majaribio ili kubaini ni mbinu ipi ina matumaini makubwa katika kudhibiti wadudu waharibifu, kuwapa wakulima maoni kuhusu namna ya kudhibiti wadudu waharibifu bila kutumia viuadudu vya kemikali kwa wingi.
- Kulinganisha taarifa zote zinazohusu teknolojia za usindikaji wa mwanzo na kubaini zile ambazo zinafaa kwa ajili ya wakulima wadogo. Kuanzisha uhusiano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).

# Idara ya Urutubishaji wa Zao



*Bw. I.K. Kullaya, Mkuu wa Idara*

Upungufu wa rutuba katika udongo unaoambatana na ukosefu wa uwezo wa kumudu mbolea za viwandani au upatikanaji wa mboji, ni sababu kubwa ya upungufu na/au upunguaji wa tija na ubora katika tasnia ya kahawa hapa Tanzania.

Idara ya Urutubishaji Zao imeanzishwa kulishughulikia suala hili na hasa kuendeleza na kukuza mfumo unaofaa wa kuthibiti rutuba ya udongo wa gharama nafuu ili kuwasaidia wakulima kufanya uamuzi wenye kuzingatia pande zote kuhusu namna watakavyodhibiti rutuba katika udongo. Idara pia itaanzisha uchanganuzi wa udongo na mimea na utaratibu wa kutoa taarifa utawaunganisha wakulima wa kahawa kwenye maabara za uchanganuzi za mikoa nchini.

**Mafanikio Makuu 2001 - 2003**

- Majaribio ya zamani yaliyorithiwa kutoka katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Lyamungu (LARTI) yalitathiminiwa na kuhifadhiwa au kurekebishwa ipasavyo. Majaribio yaliyorekebishwa yamejumuisha.
    - Tathimini ya kufaa kwa mawe ya fosfati yaliyochimbwa nchini kama mbadala wa fosiforasi iliyopo sasa ambayo inaagizwa toka nje. Ikileta mafanikio, fosfati hii ya miyamba iliyopo nchini itawapa wakulima wa kahawa unafuu mkubwa wa chanzo na upatikanaji wa mbolea ya fosforasi.
    - Kuangalia uongezaji wa kiasi cha mbolea kwa msongamano wa kahawa shambani
    - Jaribio la chokaa.
- Zaidi ya sampuli 100 za udongo kutoka kwa wakulima zilifanyiwa uchanganuzi wa vigezo halisi vya urutubishaji wa udongo. Ushauri ulitolewa kwa wakulima kuhusu namna ya kubadili mfumo wao wa kudhibiti udongo ipasavyo.
- Ubunifu mkubwa wa kupata taarifa zilizopo na utafiti kuhusu teknolojia za urutubishaji wa udongo zenye gharama nafuu ulianzishwa. Maandishi yanayoandaliwa yanajumuisha matumizi ya mbolea na mboji katika kahawa, udongo mzuri kwa ustawishaji wa kahawa na utengenezaji wa mboji kutokana na mabaki ya kahawa.
- Idara ilishiriki kikamilifu katika sikukuu ya Nanenane ya mwaka 2002 na maonyesho ya Kilimo Kilimanjaro.
- Zaidi ya wanafunzi 50 wa shule za sekondari walipewa mafunzo ya nadharia na vitendo katika vipengele vya udongo na uzalishaji wa kahawa kama sehemu yao ya mafunzo kwa vitendo, kama ilivyofanyika kwa kundi la wanafunzi 30 wa SUA. Lengo muhimu la zoezi hili, lilikuwa kuwavutia vijana katika uzalishaji wa kahawa ambao kwa hivi sasa limetawaliwa na wazee.

**Vipaumbele Vikuu 2003 – 2004**

- Kumaliza upitiaji upya wa taarifa zilizopo wa udhibiti fungamani wa udongo na rutuba katika kahawa na kuchapisha vitabu kwa ajili ya wakulima ambavyo vinaweza kutumika katika tathmini za haraka za shamba.
- Kubainisha masuala ya kufanyiwa utafiti yenye kuleta matumaini zaidi ambayo yanafaa kwa ukulima wa kahawa na mifumo ya maisha katika nchi nzima.
- Kuendelea na majaribio ya kutathmini teknolojia kwa ajili ya matumizi ya mbolea ya viwandani na mboji ili kuongeza tija na faida.
- Kuanzisha majaribio ya shambani angalau katika kanda nne za kiikolojia.
- Kuanza majaribio ya kupima mwitikio wa aina mpya iliyostawishwa katika msongamano mkubwa ambao utasaidia kutoa ushauri kwa wakulima wakubwa kuhusu faida za matumizi ya nitrojeni, fosforasi na potasiamu.
- Kuendelea na majaribio kuhusu mawe ya fosfati yanayochimbwa nchini; majaribio ambayo yanatarajia kumalizika mwaka 2008.

# Idara ya Riziki na Uhakika wa Kipato



*Mkulima mdogo wa kahawa mkoani Kagera akielezea athari za ugonjwa wa mnyauko fusari (CWD)*

Wakulima 400,000 na familia zao wanapata riziki zao kutokana na shughuli za ukulima wa kahawa Tanzania. Kuna ufahamu mdogo sana unaojulikana kuhusu sababu ambazo zinachangia katika uendelevu na mafanikio ya mifumo inayohitilafiana ya kilimo na riziki. Ili TaCRI iweze kutoa teknolojia ya maana na inayofaa, pamoja na ushauri kwa wakulima hawa wengi, ni muhimu kuelewa zaidi kuhusu mazingira ambamo wanaishi na kufanya kazi.

Idara ya Riziki na Uhakika wa Kipato ni Idara mpya iliyoanzishwa kuelezea na kuelewa uanuwai wa mifumo ya ukulima na riziki katika maeneo yanayozalisha kahawa nchini, pili kuweka vipaumbele katika vikwazo vya tija na faida na tatu, kupendekeza, kutathmini na kuendeleza suluhisho zinazowezekana.

**Mafanikio Makuu 2001-2003**

Idara hii bado iko katika mchakato wa kujiweka katika nafasi yake na itaanza utekelezaji kwenye kipindi cha miezi 12 ijayo.

**Vipaumbele Vikuu 2003-2004**

- Kuajiri mchumi na mwanasosholojia ya vijijini
- Kufanya uchunguzi wa kijamii na kiuchumi katika wilaya wakilishi ili kuboresha uelewa wa masuala yanayolikabili kundi hili muhimu la wadau.
- Kutathmini matokeo ya utafiti ili kubaini utatuzi wa kuboresha riziki za wakulima wa kahawa.
- Kutumia matokeo ya tafiti kutoa ushauri wa kiutendaji katika idara nyingine ndani ya TaCRI. Kuhakikisha kwamba shughuli za taasisi zinaendelea kukidhi mahitaji ya wakulima.

# Kitengo cha Usambazaji Teknolojia na Mafunzo

Kitengo cha Usambazaji Teknolojia na Mafunzo cha TaCRI kina mchango muhimu kama msemaji mkuu wa shughuli zote za TaCRI. Idara hii ina wajibu wa kutangaza matokeo ya utafiti wa taasisi kwa wadau wa tasnia ya kahawa kwa njia mwafaka na ya maana kwa makundi mbalimbali ya wadau. Jukumu lingine muhimu la kitengo ni kusaidia usambazaji wa aina za kahawa zilizoboreshwa kwa wakulima kukiwa na tumaini la kuwepo kwa mpango mkubwa wa kitaifa wa kupandikiza upya mikahawa katika miaka michache ijayo.



*Bw. T.S. Nzallawahe, Mkuu wa Idara*

Shabaha ni kwamba aina bora itapatikana kibiashara na kuzalisha miche kwa wastani wa vipandikizi milioni 5 kila mwaka ifikapo 2007. Inakadiriwa kwamba ugawaji wa kiasi kikubwa cha aina hizi kwa wakulima wa kahawa utaanza mwaka 2007-2008.

**Mafanikio Makuu 2001-2003**

- Bustani ya vikonyo kwa ajili ya uzalishaji wa aina mpya zilizochaguliwa imeanzishwa Lyamungu. Hivi sasa miti mama 8,500 tayari imeshapandwa. Haya ni mafanikio makubwa, ukizingatia kwamba TaCRI ilianza mwezi Septemba 2001 ikiwa na mti mmoja kwa kila aina.
- Vitengo vya Uzalishaji Kiuoto (VPU) vilivyopo Lyamungu vimepanuliwa na kujumuisha kiuoto kipya (VPU) kinachotumia gharama ndogo na nyenzo rahisi ambacho kimetathminiwa kwa ajili ya uzalishaji wa vipandikizi kwa ajili ya wakulima wadogo.
- Idara imeanzisha mpango wa mafunzo (Kufundisha Wakufunzi) ambapo watumishi wa ugani na viongozi wa vikundi vya wakulima watapata maarifa na ujuzi muhimu ambao wataueneza ujumbe wa kitaalamu hadi kwa wakulima katika ngazi za chini kabisa. Hadi hivi sasa watu 428 wameshapata mafunzo katika wilaya 12 zinazozalisha kahawa hapa nchini. Karibu wakulima 800 tayari wamepata mafunzo katika kituo kidogo cha Ugano katika Mkoa ya Ruvuma.
- Ufuatiliaji umeonyesha kwamba uzalishaji wa kahawa kivikundi umeboresha kahawa kutokana na mafunzo yaliyotolewa na

hatimaye imeongeza mapato kwa wakulima. Matokeo yake ni mvuto katika dhana ya uzalishaji kwa vikundi umeongezeka sana.

- TaCRI imepokea zaidi ya wageni 500 kutoka ndani na nje ya nchi ambao wanajumuisha wakulima, wanasayansi, wanafunzi, wabia wa wandeleo, watawala na wanasiasa.
- Mawasiliano ya mwanzo yameshafanyika na wataalamu wa kahawa wa wilaya (DCSMS) katika wilaya lengwa 12 kama wabia wa mstari wa mbele katika mkakati wa uhamishaji wa teknolojia.
- Utayarishaji wa ujumbe wa ugani uko katika hatua za mwisho kwa ajili ya kusambaza kabla ya mwisho wa mwaka.
- Mafunzo kwa ajili ya uzalishaji wa vipandikizi vya kahawa umeshaanza na kozi kubwa imeandaliwa kutolewa mwisho wa Julai 2003.
- TaCRI ilishiriki katika onyesho moja la kilimo kitaifa na maonyesho mawili ya wilaya ambapo msisitizo mkubwa ulikuwa ni kufufua tasnia ya kahawa kwa kuendeleza na kusambaza teknolojia mwafaka.

**Vipaumbele Vikuu 2003 – 2004**

- Kuunda mikakati ya mawasiliano ya muda wa kati ambayo itahakikisha utawanyaji wa ujumbe wa kitaalamu kwa wakati unaofaa na wenye kusudi maalumu kwa wadau mbalimbali.
- Kushirikiana na idara nyingine ili kupata na kutengeneza miongozo ya teknolojia ya kisasa kwa maeneo fulani muhimu itakayotawanywa kwa angalau vikundi 50 vya wakulima na mashamba makubwa 10 ifikapo katikati ya 2004.
- Kutoa nyenzo za kutolea mafunzo kuhusu vipengele vyote vinavyohusiana na uzalishaji wa kahawa na usindikaji wa mwanzo kwa ajili ya majaribio ifikapo katikati ya 2004.
- Kuendelea na Mpango wa Kutoa Mafunzo kwa Wakufunzi.
- Kuendelea na upanuzi wa bustani za miti-mama hadi kufikia miti 10,000 ifikapo mwishoni mwa 2004. Lengo ni uzalishaji wa mimea mipya 500,000 kila mwaka ifikapo 2004 kwa ajili ya kuigawa kwa wakulima ambao watakuwa wamepata changamoto ya kuanzisha bustani mama zao wenyewe kwa lengo la kupanua mradi. Lengo la mwisho ni kuzalisha vipandikizi milioni 5 kwa mwaka kwa nchi nzima ifikapo 2007.

# Uchunguzi Kifani

## Mchakato wa Uzalishaji Wa Vipandikizi Vipya vya Kahawa Bora Mahuluti



*Utunzaji wa vikonyo kwenye visanduku ilivitoe mizizi*

Moja ya jukumu muhimu la TaCRI ni utoaji na usambazaji kwa wingi wa aina bora za kahawa zinazotoa mavuno mengi, zinayostahimili magonjwa na zenye ubora wa kutosha.

Huu ni mchakato wa muda mrefu na taasisi inashughulikia changamoto hizi kwa njia zifuatazo:

**Kuchagua aina mpya za kahawa**
Kwanza kabisa, mbegu huchaguliwa na wanasayansi waboreshaji wa zao kwa kufuata sifa zinazotakiwa za kustahimili magonjwa, kutoa mavuno mengi, kuwa na punje kubwa na muonjo mzuri. Hii siyo tu inajumuisha majaribio yanayofanyika katika kituo cha utafiti cha Lyamungu, bali pia inahitaji majaribio yanayofanyika shambani ili kuona ubora wa aina mpya katika mazingira “halisi ya shamba” ikilinganishwa na aina za kibiashara zilizopo.

**Uzalishaji kwa wingi wa Aina Mpya**
Mara aina bora ya kahawa inapobainishwa, kazi kubwa hapo ni kuchapusha uzalishaji kwa wingi wa mimea kwa ajili ya usambazaji kwa wakulima wa kahawa ili waweze kuanza mchakato wa kuanza kubadilisha aina za zamani na kupanda aina mpya ambazo zina muonjo mzuri, zinastahimili magonjwa, zinatoa mavuno mengi, mambo muhimu sana katika ufufuaji tasnia ya kahawa hapa Tanzania.

**Mbinu ya ustawishaji wa Tishu**
Njia yenye ufanisi katika uzalishaji kwa wingi wa vipandikizi ni ile ya ustawishaji wa tishu. Njia hii huzalisha miti inayofanana na miti mama iliyochaguliwa kwa kutumia uoteshaji tishu (uanzishaji kiini tete kwa seli mwili). Faida ya njia hii ni kwamba inaweza kuzalisha kwa wakati uleule maelfu kwa maelfu ya vizalia kutokana na mti-mama mmoja. Kwa hivi sasa hapa Tanzania hakuna nyenzo za ustawishaji kahawa kwa tishu, ingawa TaCRI tayari imeshazalisha aina mpya zilizochaguliwa katika kituo maalumu cha ustawishaji wa Tishu huko Ufaransa (CIRAD). Kwa hivi sasa aina hizo zinafanyiwa tathmini katika baadhi ya mashamba makubwa na madogo nchini Tanzania ili kuangalia ufanisi wake katika mazingira tofauti na

kulinganisha na aina za kibiashara zilizopo. Vilevile, TaCRI kwa kushirikiana na CIRAD itajenga maabara ndogo ya ustawishaji wa tishu hapa Tanzania, kutathmini kama zile aina zote zilizoboreshwa zinaweza kuzalishwa kwa kutumia uanzishaji kiinitete kwa seli mwili na hapo baadaye kusaidia shughuli za ustawishaji wa tishu.

**Mbinu ya Vikonyo**

Kwa sasa mbinu ya kawaida ya vikonyo inatumika kuzalisha miche kwa wingi. Hekta moja ya bustani ya vipandikizi imeanzishwa Lyamungu kwa lengo la kupata miti-mama 10,000 ya hizi aina bora. Jinsi miti-mama inavyostawi na kuanza kutoa vichipuzi vipya, vipandikizi vinavunwa na kuoteshwa na kufanywa miche. Miche hii pia itachukuliwa na kutawanywa katika bustani za upili wilayani na kwenye mashamba makubwa ya vipandikizi ambapo zitazalisha miche mingi zaidi kwa ajili ya wakulima.

Bustani ya vipandikizi inatarajiwa kufikia lengo lake la miti-mama 10,000 kuzalisha vipandikizi 500,000 kwa mwaka kufikia mwishoni mwa mwaka 2004. Lengo ni kuwa na wakulima wa kahawa nchi nzima ambao wao wenyewe wataanzisha vituo vya gharama nafuu vya kuzalishia vipandikizi kutokana na miti-mama inayotolewa na TaCRI. Lengo ni kuwa na uzalishaji wa vipandikizi milioni 5 vya aina mpya kila mwaka ifikapo mwaka 2007 tutakapoanza kubadilisha miti ya kahawa inayokaribia milioni 200 inayolimwa hivi sasa nchini Tanzania.

Kwa kuwa mbinu ya ustawishaji wa tishu ni ya haraka kuliko uzalishaji wa vikonyo inatumainiwa kwamba, mbinu hii itachapusha uzalishaji wa aina mpya za kahawa. Bodi ya TaCRI inatilia hili mkazo.

## Ramani ya sehemu muhimu za kilimo cha kahawa Tanzania ikionyesha vituo vya utafiti wa kahawa na mafunzo



## Waliopiga picha:

| | |
|---|---|
| Uk. wa Mbele | Kikonyo cha kahawa: *Paul Hicks* |
| Ukurasa 1 | Mwenyekiti Mtei: *James Teri* |
| | Mkurugenzi Mtendaji Mkuu: *Nuru Ilala* |
| Ukurasa 3 | Biashara ya zao la kahawa (Amir Hamza): *James Teri* |
| Ukurasa 4 | TaCRI inaendeleza aina mpya ya kahawa inayotoa mavuno mengi na isiyoshambuliwa na magonjwa: *William Stephens* |
| Ukurasa 7 | Uchanganuzi wa wadau: *William Stephens* |
| | Ukataji mkali: *James Teri* |
| Ukurasa 9 | Dkt. Omar Kizango: *James Teri* |
| Ukurasa 10 | Bw. Deusdedit Kilambo: *James Teri* |
| | Jaribio lilokarabatiwa: *James Teri* |
| | Jaribio lililotelekezwa: *James Teri* |
| | Bw. Damian Mtenga: *William Stephens* |
| Ukurasa 12 | Dkt. Grace Chipangahelo: *William Stephens* |
| Ukurasa 13 | Bw. I.K. Kullaya: *James Teri* |
| Ukurasa 15 | Mkulima mdogo wa kahawa mkoani Kagera akielezea athari za ugonjwa wa mnyauko fusari (CWD): *James Teri* |
| Ukurasa 16 | Bw. T.S. Nzallawahe: *William Stephens* |
| Ukurasa 18 | Utunzaji wa vikonyo kwenye visanduku ilivitoe mizizi: *William Stephens* |
| Ukurasa 20 | Ramani: *Petra's Maridadi Ltd.* |

Uandishi na Uchapishaji Louisa Muir
Usanifu Petra's Maridadi Ltd.

© TaCRI, 2003



TaCRI

**TAASISI YA UTAFITI WA KAHAWA TANZANIA**
**LYAMUNGU**
S.L.P 3004, Moshi, Tanzania
Simu / Fax: +255 27 2756773
Email: tacriced@kicheko.com